TANZANIA REVENUE AUTHORITY

ISO 9001: 2015 CERTIFIED

# UTARATIBU WA KUTOA MSAMAHA WA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI (VAT) KWA MIRADI INAYOGHARIMIWA NA FEDHA ZA SERIKALI AU WAFADHILI

## UKUMBI WA
## UBUNGO PLAZA

**25 NOVEMBA,2021**

# Mawanda ya Wasilisho

- Utangulizi
- Mabadiliko ya Kipengele cha 6(2) cha Sheria ya VAT
- Msingi wa Utoaji wa Msamaha
- Kanuni za Sheria ya VAT za Mwaka 2021
- Hatua Iliyofikiwa Katika Utoaji Hati za Msamaha
- Changamoto Katika Kuomba na Kushughulikia Maombi ya VAT
- Maazimio (The Way Forward)

# 1.0 UTANGULIZI

- Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ilianzishwa nchini Tanzania July 1998 badala ya Kodi ya Mauzo (sales tax);
- VAT ilianzishwa kwa sababu kubwa tatu;
  - wigo mpana;
  - uwezo wake wa kuiletea Serikali mapato mengi na
  - Kutoegemea upande wowote katika kufanya maamuzi hasa ya kiuwekezaji (Neutrality in terms of decision affecting investment ( no cascading effect).

# 1.0 UTANGULIZI …

- Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ni kodi ya mlaji inayotozwa katika bidhaa zinazostahili kutozwa kodi, ikiwa ni pamoja na huduma, mali zisizohamishika na shughuli yoyote ya kiuchumi wakati wowote thamani inapoongezeka katika kila hatua ya uzalishaji na katika hatua ya mwisho ya mauzo.
- Kodi ya Ongezeko la Thamani inatozwa kwa bidhaa na huduma husika zinazozalishwa ndani ya nchi na pia zinazoingizwa nchini.
- Kodi ya Ongezeko la Thamani inatozwa/kukusanywa na mtu aliyesajiliwa kulipa kodi hiyo au mfanyabiashara yoyote ambaye anaweza kujirejeshea kodi kwenye manunuzi kwa kutoa kiasi hicho cha kodi kwenye kodi atakayotoza kwenye mauzo yake.
- Mlaji wa mwisho ndiyo mlipaji wa kodi

## 2. MABADILIKO YA KIFUNGU CHA 6 CHA SHERIA YA KODI YA VAT KUHUSU UTOAJI WA MSAMAHA WA VAT

- Marekebisho yaliyoishafanyika kwa ufupi hadi kufikia 2021 (VAT 1998, 2014, 2017, 2021)
  - Kabla ya 2014 -majedwali 3
    - Jedwali 1: Zero rates (items 3)
    - Jedwali 2: Exempted items (items 12)
    - Jedwali 3: Special Relief (5 persons)
  - Marebisho makubwa (revamp) Sheria ya VAT
  - Marekebisho ya kiwango cha kodi 20% - 18%
  - Marekebisho ya Kiwango cha usajili TZS 20m - 40m – 100m

## 2. MABADILIKO YA KIFUNGU CHA 6 CHA SHERIA YA KODI YA VAT KUHUSU UTOAJI WA MSAMAHA WA VAT

- Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani imefanyiwa marekebisho kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2021 ili;
  - Kumpa mamlaka kisheria Kamishana Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kutoa misamaha ya VAT (Sec.6(2)) katika maeneo yaliyoinishwa kisheria;
  - Kuongeza wigo wa kutoa misamaha ikizihusisha taasisi zisizo za Kiserikali (NGOs) Sect 6(2)(e)

# 2. MABADILIKO YA KIFUNGU CHA 6 CHA SHERIA YA KODI YA VAT KUHUSU UTOAJI WA MSAMAHA WA VAT

- Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani imebainisha kwamba, msamaha wa VAT utatolewa iwapo;
  - msamaha huo umeainishwa katika Jedwali la misamaha la Sheria ya VAT au
  - kupitia kifungu 6(2) katika Sheria hiyo.

- Kupitia Mabadiliko ya sheria ya VAT, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato ana mamlaka ya kutoa msamaha wa VAT kwa;
  - Wazalishaji wa vyandarua vyenye viuatilifu,
  - Miradi itakayogharamiwa kwa fedha za Serikali, na
  - miradi inayofadhiliwa na wahisani kupitia misaada au mikopo

  endapo mikataba baina ya Serikali na Wahisani imeweka kifungu kinachotoa msamaha wa VAT.

- Lengo ni kupunguza gharama za miradi ili kuwezesha miradi hiyo itekelezwe kwa gharama nafuu na kwa wakati kwa kutojumuisha gharama za kodi (VAT).

## 2. MABADILIKO YA KIFUNGU CHA 6 CHA SHERIA YA KODI YA VAT KUHUSU UTOAJI WA MSAMAHA WA VAT

- Kwa upande wa miradi inayogharamiwa kwa fedha za ndani za Serikali, Sheria ya VAT imeweka wazi kwa kuitaja miradi hiyo inayostahili kupata msamaha wa VAT ambayo inahusisha;
  - miradi ya Miundombinu ya Maji,
  - Usafirishaji,
  - Gesi na Nishati,
  - Ujenzi wa majengo kwa ajili ya kutoa huduma za afya au elimu kwa jamii na
  - vituo vya watu wenye ulemavu.

- Hii inamaanisha kuwa siyo miradi yote inayogharimiwa na fedha za Serikali inakidhi vigezo vya kupata msamaha wa VAT.

# 3. MSINGI WA UTOAJI WA MSAMAHA

- Kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya VAT, Sura 148 miradi inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo kupitia mikopo (Loans), au misaada (Grants), pamoja na miradi inayogharamiwa kwa fedha za Serikali, itapewa msamaha wa VAT kwa kufuata utaratibu ufuatao:
  - Maombi ya msamaha wa VAT kwa miradi inayogharamiwa kwa fedha za Serikali yatahusu tu baadhi ya miradi.
  - Maombi ya misamaha ya VAT kwa miradi ya Wizara, yawasilishwe moja kwa moja kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato.
  - Maombi ya Idara, Taasisi na Wakala za Serikali yawasilishwe kupitia Wizara mama inayosimamia Taasisi husika.
  - Maombi ya Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa yawasilishwe kupitia Mamlaka inayosimamia - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)

# 3. MSINGI WA UTOAJI WA MSAMAHA

- Msamaha wa VAT utatolewa kwenye miradi itakayogharamiwa kwa fedha za Serikali na miradi itakayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo kupitia misaada au mikopo **endapo mikataba baina ya Serikali na wafadhili imeweka sharti la utoaji wa msamaha wa VAT kwa mradi husika**.

- Msamaha utatolewa kupitia Hati ya Msamaha ambayo itabainisha bidhaa na huduma zinazosamehewa VAT, tarehe ya kuanza kutumika na kumalizika kwa msamaha husika;

- Kuweka utaratibu na masharti ya utoaji wa msamaha wa VAT ikiwemo adhabu kwa ukiukwaji wa msamaha utakaotolewa.

# 3. MSINGI WA UTOAJI WA MSAMAHA

- Msamaha utakaotolewa chini ya utaratibu huu utafutwa endapo bidhaa au huduma iliyopewa msamaha itatumika na mtu mwingine ambaye hakukusudiwa kufaidika na msamaha husika.

- Endapo msamaha uliotolewa utatumika kinyume na malengo kusudiwa, basi msamaha huo utafutwa na Taasisi iliyopewa msamaha itawajibika kulipa kodi iliyopotea kwa kuzingatia Sheria;

# 4. KANUNI YA SHERIA ZA VAT ZA MWAKA 2021

- Katika kutoa ufafanuzi wa marekebisho ya kifungu cha 6(2) cha Sheria ya VAT, iliandaliwa Kanuni ya Sheria ya VAT ya mwaka 2021 na kusainiwa na Waziri wa Fedha na Mipango tarehe 23 Septemba, 2021.
- Kanuni hizi zinajulikana kama *VAT(Exemption Management Procedures) Regulations, 2021*

- Mambo yaliyoainisha katika Kanuni hizi ni pamoja na;
  - Jinsi ya kuomba msamaha wa kodi;
  - Kuchakata na kutoa Hati za Msamaha wa Kodi;
  - Ufuatiliaji wa msamaha wa kodi uliotolewa na
  - General provissions

# 4. KANUNI YA SHERIA YA VAT YA MWAKA 2021

- **Jinsi ya kuomba msamaha wa kodi;**
  - Maombi ya msamaha wa kodi yatawasilishwa kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato kupitia Fomu Na.ITX 264.01.E;
  - Maombi yawasilishwe kwa Kamisha Mkuu miezi 2 kabla ya mradi husika kuanza kutekelezwa;
  - Maombi ya misamaha ya VAT yanapaswa kuwasilishwa Mamlaka ya Mapato yakiambatanishwa na nyaraka zifuatazo;
    (i) Mikataba ya ufadhili wa mradi (mkopo au msaada) uliosainiwa kati ya Wizara ya Fedha na Mipango na Mfadhili;

# 4. KANUNI YA SHERIA YA VAT YA MWAKA 2021

- **Jinsi ya kuomba msamaha wa kodi;**

(ii) Mkataba wa utekelezaji wa mradi uliosainiwa kati ya Afisa Masuuli na Mkandarasi/Mshauri elekezi;

(iii) Kuonesha orodha ya vifaa, bidhaa na huduma zinazoombewa msamaha, mahali ambapo huduma, bidhaa au vifaa vinaponunuliwa (nje au ndani ya nchi) kwenye Fomu Na. ITX 264.01.E;

(iv) Kwa miradi ambayo ilikwisha pata hati ya msamaha (GN) awali muombaji anapaswa kujaza fomu Na. ITX 282.01.E ili kuonesha matumizi ya msamaha huo na kiasi cha vifaa kilichobaki;

# 4. KANUNI YA SHERIA YA VAT YA MWAKA 2021

- **Jinsi ya kuomba msamaha wa kodi;**

(v) Nakala ya barua kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliyohakiki mikataba ya utekelezaji baina ya mkandarasi na Wizara au Taasisi husika kwa mikataba inayostahili kuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410;

(vi) Uthibitisho wa kimaandishi kutoka kwa Wizara au Taasisi yenye mradi, kuthibitisha kwamba ukokotoaji wa gharama za mradi haukuhusisha VAT;

(vii) Uthibitisho wa muhuri na saini kutoka kwa Wizara au Taasisi yenye mradi, kuthibitisha kwamba orodha ya vifaa au Huduma inayoombewa msamaha ni vile tu vitakavyotumika moja kwa moja kwenye mradi

# 4. KANUNI YA SHERIA YA VAT YA MWAKA 2021

- **Kuchakata na kutoa Hati za Misamaha ya Kodi;**
  - Msamaha utatolewa tu pale Kamishna mkuu atakapokuwa ameridhia baada ya kupitia nyaraka muhimu na kujiridhisha kuwa zinafaa;
  - Wakati wa mapitio ya nyaraka, Kamishna Mkuu anaweza kuomba taarifa zingine kutoka kwa mwombaji au Wizara husika;
  - Maombi ya msamaha yanaweza kukubaliwa au kukataliwa kulingana na uchambuzi na uchunguzi uliofanyika na kama maombi yatakataliwa basi Kamishna Mkuu anawajibika kutoa sababu za kukataa na kama yatakubalika basi itatolewa Hati ya Msamaha wa kodi kupitia Form No. ITX 281.01.E

# 4. KANUNI YA SHERIA YA VAT YA MWAKA 2021

- **Kuchakata na kutoa Hati za Misamaha ya Kodi;**
- Msamaha wa kodi utatolewa ndani ya siku 30 tangu maombi yalipowasilishwa kwa Kamishna Mkuu
- Hati ya Msamaha ina taarifa muhimu zikiwemo;
  Jina la mnufaika wa mradi, mkandarasi, tarahe za kutolewa na kuisha hati, bidhaa au huduma zilizoombewa msamaha, n.k.
- Mwombaji aliyepata Hati ya Msamaha ataendelea na utaratibu wa kutumia bidhaa hizo Form Na. ITX 265.01.E .

# 4. KANUNI YA SHERIA YA VAT YA MWAKA 2021

- **Ufuatiliaji wa msamaha wa kodi uliotolewa**
  - Kamishina atafanya ukuguzi wa matumizi ya msamaha wa kodi uliotelewa muda wowote atakaoona unafaa;
  - Katika kufanya ukaguzi Kamishana atapitia nyaraka za ununuzi wa vifaa au huduma na matumizi yake kuona kama vinaendana na msamaha uliotelewa;
  - Endapo Kamisha atabaini ukiukwaji wa msamaha, basi atalazimika kukadiria na kukusanya Kodi ya Ongezeko la Thamani iliyopotea kutokana ukiukwaji wa matumizi ya msamaha huo.

# 5. HATUA ILIYOFIKIWA KATIKA UTOAJI HATI ZA MSAMAHA WA KODI (HADI 30 OCT)

| Na | Mkoa | Tar Kupokea | idadi ya Mikataba | Iliyidhinishwa | Hati | Iliyo bado | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | DAR ES SALAAM | 27.09.2021 | 2 | 3 | 3 | | |
| 2 | PWANI | 27.09.2021 | 2 | | | 2 | WIP |
| 3 | MWANZA | 27.09.2021 | 14 | | | 14 | DOCS NOT SUB |
| 4 | DODOMA | 27.09.2021 | 1 | | | 1 | WIP |
| 5 | TANGA | 27.09.2021 | 1 | 1 | 1 | | |
| 6 | DODOMA | 27.09.2021 | 3 | | | 3 | WIP |
| 7 | MOROGORO | 27.09.2021 | 2 | 1 | 1 | | WIP |
| 8 | KATAVI | 27.09.2021 | 3 | 3 | 3 | | |
| 9 | TABORA | 13.10.2021 | 25 | 25 | 25 | | |
| 10 | GEITA | 13.10.2021 | 22 | 22 | 22 | | |
| 11 | DODOMA | 13.10.2021 | 16 | 16 | 16 | | |
| 12 | MBEYA | 13.10.2021 | 15 | 15 | 15 | | |
| 13 | KAGERA | 13.10.2021 | 7 | | | 7 | WIP |
| 14 | SONGWE | 01.11.2021 | 6 | | | 6 | WIP |
| 15 | RUVUMA | 01.11.2021 | 26 | 26 | 26 | | |
| 16 | SHINYANGA | 13.10.2021 | 26 | 26 | 26 | | |
| 17 | KATAVI | 13.10.2021 | 21 | 21 | 21 | | |
| 18 | SIMIYU | 13.10.2021 | 17 | 17 | 17 | | |
| 19 | SINGIDA | 13.10.2021 | 17 | 14 | 14 | 3 | WIP |
| 20 | KIGOMA | 13.10.2021 | 13 | 13 | 13 | | |
| 21 | MARA | 13.10.2021 | 13 | | | 13 | WIP |
| 26 | RUVUMA | | 17 | 17 | 17 | | |
| 27 | PWANI | 13.10.2021 | 2 | | | 2 | WIP |
| | **TOTAL** | | **271** | **220** | **220** | **51** | |

# 5. HATUA ILIYOFIKIWA KATIKA UTOAJI HATI ZA MSAMAHA WA KODI (1 – 19 Nov 2021)

| Na. | Mkoa | Idadi ya Mikataba | Tarehe ya kupokelewa | Mikataba iliyoidhinishwa | Hati Imetolewa | Hati Bado Kutolewa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SONGWE | 6 | 01.11.2021 | 6 | | 6 | PRINTING PROCESS |
| 2 | RUVUMA | 26 | 01.11.2021 | 26 | | 26 | PRINTING PROCESS |
| 3 | KAGERA | 32 | 08.11.2021 | | | 32 | WIP |
| 4 | LINDI | **25** | 08.11.2021 | | | 25 | WIP |
| 5 | MTWARA | 37 | 08.11.2021 | | | 37 | WIP |
| 6 | TANGA | 42 | 08.11.2022 | | | 42 | WIP |
| 7 | SHINYANGA | 24 | 08.11.2023 | 24 | | 24 | PRINTING PROCESS |
| 8 | KIGOMA | 7 | 10.11.2021 | 7 | 7 | | |
| 9 | SIMIYU | 6 | 10.11.2022 | 6 | 6 | | |
| 10 | RUKWA | 17 | 10.11.2023 | 17 | | 17 | PRINTING PROCESS |
| 11 | NJOMBE | 12 | 10.11.2024 | | | 12 | PRINTING PROCESS |
| 12 | MOROGORO | 37 | 10.11.2025 | | | 37 | WIP |
| 13 | MANYARA | 2 | | 2 | 2 | | |
| 14 | SHINYANGA | 26 | | 26 | | 26 | PRINTING PROCESS |
| **Jumla** | | **299** | | **114** | **15** | **284** | |

# 6. CHANGAMOTO KATIKA KUSHUGHULIKIA MAOMBI YA MSAMAHA WA VAT

Kumekuwa na changamoto kwenye utekelezaji wa Sheria hii kutokana na baadhi ya vipengele kutoeleweka vema na watekelezaji wa miradi kama ifuatayo:

- Miradi kutokidhi vigezo vya kupata msamaha wa VAT kwa mujibu wa Sheria ya VAT kutokana na baadhi ya mikataba kusainiwa bila idhini ya Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha (Wizara ya Fedha na Mipango) kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Misaada, Mikopo na Dhamana ya mwaka 1974 pamoja na marekebisho yake.

- Baadhi ya mikataba iliyosainiwa kutokuwa na vipengele vinavyotoa msamaha wa kodi kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani.

# 6. CHANGAMOTO KATIKA KUSHUGHULIKIA MAOMBI YA MSAMAHA WA VAT

- Orodha ya vifaa vinavyowasilishwa kwa ajili kuombewa msamaha kutokuwa na uhusiano wa moja kwa moja kwenye utekelezaji wa mradi kulingana na matakwa ya sheria ambapo baadhi ya Wizara zimekuwa zikiwasilisha maombi ya msamaha kwa ajili ya vitendea kazi na mali binafsi za wakandarasi.

- Kucheleweshwa kwa maombi ya msamaha wa VAT ambapo baadhi ya maombi yamekuwa yakiwasilishwa wakati vifaa vimeshafika bandarani;

# 7. MAAZIMIO (THE WAY FORWARD)

- Kuendesha vipindi vya mafunzo kama hiki wakati wa kujifunza mfumo wa kuomba msamaha wa kodi ili kuongeza uelewa na kuepuka makosa yanayosababisha ucheleweshaji wa kutoa msamaha
- Ifikapo mwezi Februari, 2022 Kuanza kutumia mfumo ili kuondokana na kubeba mizigo ya makablasha ikiwemo mikataba
- Wakati wa kipindi hiki kabla ya kuanza kutumia mfumo, tunaomba kupatiwa soft copy ya orodha ya wakandari na vifaa ili iwe rahisi kuandaa Hati za Msamaha
- Kuimarisha ushirikiano wa karibu na kurekebisha changamoto zilizotajwa hapo juu na zingine zinazoweza kujitokeza ili kurahisisha zoezi la utoaji Hati

# ASANTENI SANA

*“Pamoja Tunajenga Taifa Letu”*